Moyo Wenye Huruma

(A Heart Of Compassion)

Na

Alex S. Silvester

Moyo Wenye Huruma

(A Heart Of Compassion)

Na

Alex S. Silvester

Oktoba 25, 2018

Moyo Wenye Huruma

Wenyechuki:

Wapo wengi katika ulimwengu wanaochukia ukweli. Wanachukia matendo mema. Wanachuki dhidi yaw engine. Ni kweli kwamba kuna vitu ambavyo vinapaswa kuchukiwa (Mit. 6:16-19), lakini haya ni mambo yanayofanya kazi kinyume na mema na haki; zinachukiwa kutokana na mvuto wao wa uharibifu. Ukristo unatafuta kupokelewa kwa kujikubali na wengine pia, ikituomba kutazamia mema, tarajia mema, na kufanya kazi kwa ajili ya mema. Hisia iliopo upande mwingine itokanayo na chuki ni huruma.

Huruma ni uwezo wa kuwa na tabia ya mwitikio katika mateso au hali ya mwingine, ikijumuisha wale ambao matendo yao binafsi yamewasababishia matatizo. Huruma unamruhusu mtu kushiriki mateso au hisia ya mwingine kwa sababu ya ubinadamu wetu na kwa sababu ya uwezekano wa kuteseka kama wao. Na huruma unauwezo wa kutuliza hisia zetu wenyewe, hasa ya hasira au maombolezo, katika uso wa makosa, kosa na dhambi za wengine, na kuchukuliana nao kwa taratibu, tukichukia dhambi. Ninaamini kwamba hii ndio aina ya roho alionao ndugu yetu Ellis; nilimfaham mwaka 2012 alipokuwa Afrika akifundisha na kuhubiri Injili kulingana na misingi ya maandiko matakatifu. Akituonyesha mafundisho sahihi niligundua kwamba tulikuwa tunaongozwa vibaya na kupotoshwa na mafundisho ya wale wanaojiita wakristo wa kisasa kwa sababu wanaweka sheriaa pasipo na sheria. Hasa katika ushirika wa meza ya Bwana. Mungu wetu na amuweke na kumtunza katika maisha haya kwa sababu kanisa linawahitaji watu kama hao.

Yesu mwenyewe alionyesha aina hii ya huruma kwa watu waliokuwa wakiteseka katika matatizo tofauti. Mathayo 9:36-38 inamwonyesha akiwahurumia wale waliohitaji mwongozo wa kiroho na kitabia katika maisha yao – "*Na alipowaona makutano aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji. Ndipo alipowaambia wanafunzi wake, mavuno ni mengi lakini watenda kazi ni wachache. Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno yake.*" Kuchanganyikiwa kiroho ni kuchanganya maana ya maisha na jinsi mtu anapaswa kuishi. Bwana aliwahurumia watu kama hao.

Pia aliwaweka sawa wale walioteseka na magumu ya miili na kutoweza. Mara zote Yesu alichukua muda akiongelea magonjwa na shidaa zilizowakabili watu wa taifa lake, "*Yesu akatoka akaona mkutano mkuu, akawahurumia, akawaponya wangonjwa wao.*" (Mat. 14:14). Bila

shaka miujiza hii ili wezesha nafasi ya kuhubiri Injili, lakini angeweza kufanya mazingaombwe na maajabu ili kuonyesha uwezo wake; aliamua kuonyesha uwezo wake sio kwa mazingaombwe, lakini kwa ishara na matendo ya huruma. Pia alishughulikia mahitaji ya kimwili, kama kuwalisha maelfu katika, "*Yesu akawaita wanafunzi wake akasema nawahurumia mkutano, kwa kuwa yapata siku tatu wamekaa pamoja nami, wala hawana kitu cha kula, tena kuwaaga wakifunga sipendi, wasije wakazimia njiani.*" (Mat. 15:32). Hataivyo hakuruhussu tukio hilo lipite bila kukubali tukio la ndani ya kile alichokifanya na ambacho angefanya (Yohana 6). Kupitia mfano wa Msamaria mwema aliwafundisha kuwajali wengine. "*Lakini Msamaria mmoja katika kusafiri kwake alifika hapo alipo; na alipomwona alimhurumia,*" (Luka 10:33). Alitoa faraja na msaada kwa wale waliowapoteza ndugu zao, kama familia ya Yairo. "*Akaja mtu mmoja katika wakuu wa sinagogi, jina lake Yairo; hata alipomwona akaanguka miguuni pake, akimsihi sana akisema, Binti yangu mdogo yu katika kufa; nakuomba uje uweke mkono wako juu yake apate kupona na kuishi. Akaenda pamoja naye, mkutano mkuu wakamfuata, wakimsongasonga. Na mwanamke mmoja mwenye kutoka damu muda wa miaka kumi na miwili, na kuteswa mengi kwa mikono ya matabibu wengi, amegharimiwa vitu vyote alivyo kuwa navyo, kusimfae hata kidogo bali hali yake ilizidi kuwa mbaya aliposikia habari zaa Yesu, alipita katika mkutano kwa nyuma, akaligusa vazi lake; maana alisema nikiyagusa mavazi yake tu nitapona. Mara chemchemi ya damu yake ikakauka, naye akafahamu mwilini mwake kwamba amepona msiba ule. Mara Yesu hali akifahamu nafsini mwake kwamba nguvu zimemtoka, akageuka katika mkutano akasema , ni nani aliyenigusa mavazi yangu? Wanafunzi wake wakamwambia je wawaona makutano wanavyokusongasonga nawe wasema, ni nani aliyenigusa? Akatazama pande zote ili amwone yule aliyelitenda neno hilo. Na yule mwanamke akaingiwa na hofu na kutetemeka akijua lililompata akaja akamwangukia, akamweleza kweli yote.*" (Marko 5:22-33). Na mjane huko Naini. "*Baadaye kidogo alikwenda mpaka mji mmoja uitwao Naini na wanafunzi wake walifuatana naye pamoja na mkutano mkubwa. Na alipokaribia lango la mji hapo palikuwa na maiti anachukuliwa nje, ni mwana pekee wa mamaye ambaye ni mjane, na watu wa mjini wengi walikuwa pamoja naye. Bwana alipomwona alimwonea huruma, akamwambia usilie.*" Hii inatukumbusha maneno ya Paulo, " *Furahini na wafurahio, lieni na waliao.*" (Rum. 12:15).

Hata kama hakuwajibika kufanya hivyo, alikuwa mwenye huruma na aliyewajali wale walioteseka kutokana na madhara ya dhambi zao. Wakati wengine wangesema umaarufu wetu, "Umetengeneza kitanda chako." Sasa kilalie! Au "Umepata ulichotafuta," Yesu alitoa mfano wa bwana anayesamehe (Mat. 18:27-33). Hakutoa udhuru kwa kufanya

kosa, bali alitaka watu wapate njia ya kutoka dhambini waje katika maisha ya haki. Mfano wa mwana mpotevu ilisemwa kwa kusudi la kuonyesha mapenzi ya Mungu ya kusamehe mwenye dhambi anayeomba msamaha.

Aihitaji uwezo maalum ili kuweza kuwa anayechukia. Aihitaji ukuaji ili kuweza kushughulikia udhaifu na kutokuwa makini kwa wengine. Lakini zaidi inahitajika katika kuzungumza na wengine kwa njia ya huruma. Tunapaswa kuchukua muda katika kuwajali wengine, kama katika mfano wa Msamaria Mwema. Tunapaswa kukubali utu wetu wenyewe. Watu wanaombolezaa na wanahitaji bega ili waweze kuegemea wanapolia. Wanahitaji mtu aendane na vitu hivyo ambavyo ni ya lazima lakini hutisha. Lazima tuwe tayari kuwasaidia wale waliokosea katika njia sahihi, ama kutoa heshima zetu kwa kilicho sahihi, au kushindwa kuwahudumia waliopotea. Kwa njia hizi tunaiga uasili uliotiwa roho wa Yesu tunapotafuta mazuri, tarajia mema, na kufanya kazi kwa mema. Tukitimiza wito wetu kama wahubiri na waalimu wa neno la Mungu.

Alex Sadat Silvester